

*Mulika, Na. 43 (2), 336-350
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Uchunguzi wa Mtagusano baina ya Hisia na Motifu: Mifano kutoka Tamthilia ya Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe

Winifrid Mligo¹

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Aldin Mutembei²

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

na

Ramadhan Thomas Kadallah³

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.8>

Ikisiri

Motifu ni mionganini mwa vipengele vilivyo chunguzwa kwenye matini za kifasihi andishi kwa mielekeo mbalimbali kama vile kuitumia kama nadharia ya uchambuzi na kama dhana ya uchambuzi. Licha ya tofauti za kimielekeo katika uchunguzi wa motifu, msingi wa tafiti hizo unatambua kuwa motifu ni kipengele radidi katika matini husika. Kwa kuwa matendo ya wahusika ndiyo yenye kuibua hali ya kujirudiarudia kwa jambo, kipengele cha wahusika kimeonekana kuhusishwa kwa karibu na motifu. Hata hivyo, ingawa tafiti na mawazo ya wataalamu hayahitilafiani kuhusu msingi wa utambuzi wa motifu, sababu inayachochea kujirudiarudia kwa vijenzi vinavyoijenga/vinavyoibua motifu hazipo bayana. Kwa hiyo, kwa kuzingatia mwelekeo wenye kuichambua motifu kama kijenzi tegemezi, utafiti huu ulifanyika ili kuchunguza vichocheo vyenye kukifanya kijenzi husika kijirudie kiasi cha kuibua motifu. Ili kutimiza lengo hilo, data zilikusanywa katika tamthilia ya *Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe* kwa kutumia mbinu ya usomaji matini huku uchambuzi wa data ukiongozwa na Nadharia ya Rasa. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba hali ya kujirudiarudia kwa jambo huchochewa na hisia za wahusika; hivyo, hisia na motifu hukamilishana.

1.0 Utangulizi

Binadamu ni mionganini mwa viumbe wengi wanaoishi katika ulimwengu ingawa kuna tofauti kadha zinazomtofautisha na viumbe wengine. Mionganini mwa jambo linalomtofautisha yeye na viumbe wengine ni mtindo wa mawasiliano. Viumbe hai

¹ Baruapepe: winifridmligo140@gmail.com

² Baruapepe: kaimutembei@gmail.com

³ Baruapepe: kadallahr@gmail.com

wote huwasiliana baina ya jamii zao wenyewe na jamii zingine lakini aghalabu binadamu hutumia lugha kuwasiliana (Haldane, 1992). Kuna namna mbalimbali za mawasiliano yenye kutumia lugha, yaani lugha ya kisanaa na isiyo ya kisanaa (Mulokozi, 2017). Makala haya yanaangazia matini yenye kilongo kilichowasilishwa kisanaa, yaani kiubunifu katika matini ya fasihi andishi. Kigezo kuhusu msingi wa matini kupewa kipaumbele ni kwa kuwa vigezo vingine kama vile mtindo wa lugha vinaleezwa kutotofautiana sana katika matini za kiubunifu na zisizo za ubunifu (Benjamin, 2012). Inaleezwa kwamba zipo sababu mbalimbali zenyne kumsukuma msanii kutunga na kuwasilisha matini husika katika jamii (Mbenna, 1970). Mionganoni mwa sababu inayomsukuma mwanajamii kuamua kulifinyanga tukio husika, kisha kuliwasilisha tena kiubunifu ni kuguswa zaidi na jambo fulani (Mohamed, 1995; Hogan, 2011). Jambo hilo linaonesha kwamba ujumbe wa matini husika ya kifasihi unapatikana kwenye hisia za wawasilishaji. Kadhalika, Hogan (2011) anafafanua kwamba mara nyingi hisia zinapotumika kuwasilishia matini husika huwa katika mtindo wa kujirudiarudia ili kukazia wazo husika. Mawazo haya ya Hogan (2011) yanaelekeana na ya Mutembei (2012) hasa anapoeleza kwamba ikiwa tukio husika katika matini ya kifasihi linawasilishwa kwa kujirudiarudia, humfanya mchambuzi aongeze umakini wa kutafuta sababu na maana ya kipengele husika kuchomoza zaidi ya vingine. Wataalamu wamekiita kipengele husika chenye kujitokeza kwa kujirudiarudia kuwa ni motifu (Senkoro, 1997; Lubbungu, 2011; wa Mutiso, 2012; Morgan, 2015). Kimsingi, mawazo ya wataalamu yameonesha kwamba kuna uhusiano baina ya motifu na uchomozaji wa kipengele fulani katika matini za kifasihi. Kutokana na ukaribu baina ya dhana ya uchomozaji na hisia katika kuibua motifu, makala haya yamechunguza mtagusano baina ya motifu na hisia.

2.0 Motifu

Motifu ni mionganoni mwa vipengele vilivyoshughulikiwa kwa kiasi kikubwa kwenye uwanja wa fasihi. Wataalamu waliochunguza kuhusu motifu katika uwanja wa fasihi hawahitilafiani kuhusu dhana ya motifu kwamba ni hali au jambo linalojirudiarudia katika matini husika (Senkoro, 1997; Lubbungu, 2011; wa Mutiso, 2012; Morgan, 2015; Mulokozi, 2017; Mung'aya; 2018; Lema, 2018; Sosoo 2019). Inafafanuliwa kwamba ujirudiaji wa hali au jambo huweza kuwa kwa namna iliyo wazi au namna fiche (Lubbungu, 2011; Morgan, 2015; Lema, 2018). Kutokana na kuwapo kwa hali ya ujirudiajirudiaji wa baadhi ya vipengele katika matini za kifasihi, wataalamu wameweza kubainisha aina mbalimbali za motifu. Mionganoni mwa motifu zinazotajwa kujitokeza katika matini za kifasihi kwa kiasi kikubwa ni motifu ya safari, motifu ya namba na motifu ya wema na ubaya kwa kutaja baadhi (Senkoro, 1997; Lubbungu, 2011; wa Mutiso, 2012; Morgan, 2015; Mulokozi, 2017; Mung'aya; 2018; Lema, 2018).

Kwa hiyo, licha ya wataalamu kubainisha aina mbalimbali za motifu, imeonekana kuwa motifu iliyoshughulikiwa kwa kiasi kikubwa ni ya safari. Mathalani,

imeonekana kuwa kuna kufanana kwa mawazo baina ya Senkoro (1997), Lubbungu (2011) na Lema (2018) kuhusu motifu ya safari. Katika ufanuzi wao wanaeleza kwamba motifu hiyo ya safari inaweza kuwa kitendo cha mhusika kutoka eneo moja la kijiografia kwenda jingine au inaweza kuwa safari ya kisaikolojia. Lubbungu (2011) anafafanua zaidi kwamba ipo motifu ya mhusika kusafiri kiimani, yaani anapokuwa mfuasi wa dini fulani huanza safari ya kuyazingatia na kuyafuata, mara kwa mara, mafundisho ya dini husika.

Morgan (2015) anaeleza kwamba motifu inaweza kujitekeza kwa njia iliyobayana au kwa njia ya ishara. Anachoeleza Morgan (2015) hapa ni kwamba uradidi wa kipengele husika katika matini unaweza kuwa dhahiri kwa kujirudia kwa namna ileile au ukawa kwa njia isiyo dhahiri ingawa hurejelea jambo lilelile. Hata hivyo, Morgan (2015) anatahadharisha kwamba si kila kinachojirudia katika matini husika huwa motifu. Hii ni kwa kuwa baadhi ya masuala ya kuzingatia katika utambuzi wa kinachojirudia kuwa motifu ni upya wake katika mtiririko husika (Morgan, 2015). Kigezo kingine kinachotajwa na Morgan (2015) ni kuhakikisha kuwa kuna ushikamani wa vipengele vinavyojirudia kiasi kwamba vikiwekwa pamoja vitakuwa na mwangwi unaoelekeana. Kwa kuzingatia vigezo tajwa, ni wazi kwamba kila kipengele chenye mwangwi unaojirudia huibua dhamira ya kimotifu.

Kuhusu hali ya kipengele husika kujirudiarudia, kumekuwa na mjadala kwamba kipengele husika kijirudie mara ngapi ili kukidhi sifa ya umotifu. Jambo hilo linawekwa bayana zaidi na Morgan (2015) anaposema kwamba hakuna idadi maalumu ya ujirudiaji wa kipengele husika ili kiweze kuwa motifu. Morgan (2015) anaeleza kwamba jambo la kuzingatia ni kuhakikisha ujirudiaji huo katika matini husika ni toshelevu na wenye kurejelea jambo moja. Kwa hiyo, mawazo ya wataalamu yanaonesha kwamba jambo la muhimu katika uibuzi wa motifu ni ujitekezaji wa mara kwa mara wa kipengele husika bila kuzingatia msingi wa kitakwimu.

Inaelezwa kwamba kipengele husika kinapojirudiarudia huvuta makini ya mchambuzi matini kiasi cha kuiuliza kwa nini jambo hili limejitekeza tena na tena (Mutembei, 2012). Kitendo cha kipengele husika kujirudia mara kadha katika matini husika ndicho kinachoibua tararuki⁴ kwa mchambuzi wa matini kiasi cha kumsukuma aibue maswali yenye kumtafakarisha (Mutembei, 2012). Kupitia maswali ya mchambuzi, ndipo huanza safari ya kuutafuta ujumbe unaokusudiwa kupitia kipengele husika (Lubbungu, 2011; Lema, 2018). Kadhalika, inaelezwa kwamba kipengele chochote katika matini chenye uwezo wa kuibua tararuki kwa mchambuzi huwa ni kipengele cha kimchomozo (Mutembei, 2012). Ingawa

⁴ Katika makala haya, inapotajwa hali ya mchomozo na tararuki inarejelea mwitiko wenye kufumbata hisia.

makala haya yamezingatia mwitiko wa wahusika katika matini husika, ni wazi kwamba kuna uhusiano wa karibu baina ya motifu na hali ya kitaharuki yenye mchomozo unaoambatana na hisia. Hivyo, katika kipengele kinachofuata tumeeleza kuhusu dhana hiyo ya mchomozo.

3.0 Mchomozo

Hii ni istilahi inayotokana na kitenzi “chomoza”, yaani tokeza au ibuka kutoka kwenye hali ya kutoonekana (BAKITA, 2022). Fasili ya BAKITA (2022) licha ya kuonesha ughafla wa kutokea kwa hali au jambo, kwa maoni yetu, hali ya kutoonekana haifungamani bayana na hali ya kuchomoza. Kwa umahususi, Leech (2008) na Mutembei (2012) wanafafanua dhana ya kuchomoza wakiihusisha na matini za kifasihi kwamba ni taharuki au ukiushi wa vitushi, vitu, hali na kadhalika, yaani kuna kimoja kinakiuka mpangilio husika kiasi cha kufanya kiwe na sifa za ziada kuliko vingine. Mawazo ya Leech (2008) na Mutembei (2012) yanaonekana kuwa bayana zaidi kuhusu dhana ya kuchomoza kwa kuwa yanaonesha mchomozo unahusiana na hali isiyotarajiwa. Kwa kiasi fulani, fasili ya mchomozo kadiri ya Leech (2008) na Mutembei (2012) ni angavu kuliko ile ya BAKITA (2022) japo yaelekeea wanatumia mkabala wa mwitiko wa msomaji pekee ilhali ipo mikabala mingine kama vile wenye kuichambua matini isiyohusisha mwitiko wa msomaji wala wa mchambuzi (Abrams, 1953). Wakati wataalamu wakionesa kutambua nafasi ya mwitiko hasa wa kitaharuki katika uwanja wa fasihi, wapo baadhi ya wataalamu wanaopinga kuzingatia hali ya taharuki katika matini za kifasihi. Mathalani, yakisasanywa mawazo ya Brecht (1957), Mounce (1980), Kezilahabi (1993), Mohamed (1995) na Boal (2008), yanaonesha kwamba mwitiko wowote wa kitaharuki wenye kuchochewa na matini ya kifasihi haufungamani na mantiki na hali ya uhakikifu.

Msingi wa madai ya wataalamu tajwa unajengwa kutokana na sababu kwamba taharuki huchochewa na hisia ambazo ni vigumu kuzichambua kutokana na utelezi wake (Mohamed, 1995). Ingawa baadhi ya wataalamu wanaonesha wasiwasi wa kuipa nafasi ya kuichambua hali ya kitaharuki katika matini za fasihi ikiambatana na hisia, makala haya hayaungi mkono mtazamo huo kwa kuwa inaelezwa kwamba hisia ndio msingi wa kutungwa kwa matini ya kifasihi (Mbenna, 1970). Hivyo, kutokana na dhana ya taharuki na hisia kuwa karibu na ile ya kuchomoza kama ilivyoelezwa na Leech (2008), Mutembei (2012) na BAKITA (2022), ni wazi kwamba mwitiko wa kitaharuki unaweza kuchunguzwa kuitia wahusika katika matini husika (Abrams, 1953).

Zaidi, msisitizo kuhusu nafasi ya mchomozo katika uwanja wa fasihi unawekwa na Leech (2008) anayeeleza kwamba mtindo wa kiufundi unaowasilisha jambo husika kwa kutumia lugha ya sanaa ndio wenye kufanya kilongo husika kiwe na uzito wa kiujumi. Mawazo ya Leech (2008) hapa yanaonesha kwamba upo uhusiano wa karibu baina ya ujumi wa kisanaa na hali ya mchomozo. Hali hii

inatokana na sababu kwamba, ikiwa jambo husika linawasilishwa bila ufundi wowote, kuna uwezekano mkubwa wa kumchosha msomaji mwenye kuichambua matini husika kutokana na kutamalaki kwa hali ya ukawaida. Hivyo, upya, ukengeushi na taharuki ni masuala ya msingi yenyе kumfanya mchambuzi atagusane na matini husika. Mchambuzi anapokuwa karibu na matini husika, humfanya aongeze juhudhi za kutafuta maana ya matini husika. Hii ni kama anavyoeleza van Dijk (2008) kwamba muktadha ni mhimiili muhimu wenye kumwezesha mchambuzi kung'amu jambo linalowasilishwa. Kwa mantiki hii, ni wazi kwamba jambo husika linapowasilishwa kwa kujirudiarudia humfanya mchambuzi ajiulize sababu ya ujirudiaji wake hatimaye kutafuta maana kulingana na muktadha wa kipengele husika. Pamoja na ukweli huo, wataalamu hawaweki bayana kuhusu nini kinachofanya kijenzi husika kijirudierudie. Kwa hiyo, suala hilo ndilo lililosughulikiwa katika makala haya.

4.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Data zilikusanywa kwa kusoma tamthilia teule kisha kubaini vipengele radidi vilivyojitokeza kimchomozo ambavyo hubeba hisia. Sehemu ya matini ambayo wahusika walionesha mwitiko wa kimchomozo zilikolezwa wino kama inavyoonekana katika uwasilishaji wa data. Mwongozo wa utambuzi wa hali ya kimchomozo wakati wa ukusanyaji wa data na ufanuzi wake uliongozwa na Nadharia ya Rasa. Nadharia hii iliasisiwa na Bharata Muni wa India kupitia andiko la *The Natyashastra* mnamo karne ya 2 K.K. Katika makala haya, imetumika misingi miwili pekee kutoka kwenye hiyo. Msingi wa kwanza unaongozwa na dhana ya *vibhavas*, yaani katika matini za kisanaa wahusika hutenda au kutamka maneno yenyе kusababisha mwitiko kwa wahusika wengine. Msingi wa pili unaongozwa na dhana ya *anubhavas* inayofafanua kwamba matendo au maneno ya wahusika husababisha wahusika wengine waoneshe miitiko au taharuki kwa namna mbalimbali iliyo wazi kama vile matamshi ya mihemko, mjongeo wa ghafla wa viungo vya mwili, ishara kupitia uso, yaani kukunja sura, kucheka na kulia. Kwa hiyo, Nadharia ya Rasa inaeleza kwamba kinachosababisha mhusika kubadilika au kufanya jambo tofauti na matarajio ya mhusika mwingine ni hisia. Kinachoelezwa hapa ni kwamba *vibhava* ni chanzo chenyе kusababisha mwitiko na *anubhava* ni matokeo au udhihirisho wa *vibhava*. Hivi ni kusema kwamba, kila mwitiko wa mhusika ni dhihirisho la hisia fulani.

Kadhalika, Nadharia ya Rasa inafafanua kwamba kila *vibhava* husababisha aina mbalimbali za hisia kama vile hisia za mapenzi, furaha, woga, hasira, chuki na huzuni. Zaidi, nadharia hii inaeleza kwamba hisia ni hali ya asili ambayo kila mmoja anayo ingawa huhitaji vichocheo vya kuifunua hisia husika. Kutokana na kubadilikabadilika kwa vichocheo yenyе kuamsha hisia, ndio sababu ya hisia husika kujitokeza kwa muda mfupi kisha kutoweka kwa ajili ya kupisha kutokea kwa aina nyingine ya hisia. Kinachoelezwa hapa ni kwamba, hisia hujitokeza kwa kujirudiarudia. Kwa ufupi, Nadharia ya Rasa ilituongoza katika kubaini hisia

radidi kwa wahusika katika hali ya mtoano, yaani mwitiko husika wa kihisia kujitokeza kwa kipindi fulani kisha kupisha mwitiko mwingine.

Kwa jumla, msukumo wa kutumia Nadharia ya Rasa katika utafiti huu ultokana na mawazo ya msingi ya nadharia hii kwamba hisia ni mwitiko wenye kujirudiarudia. Hii ni kwa kuwa mawazo ya msingi ya dhana ya motifu vilevile yanaeleza kwamba inatokana na kujirudiarudia kwa kijenzi husika. Jambo hilo ndilo hasa lililotufanya tuchunguze ikiwa kinachorudiwarudiwa katika matini na kujulikana kama motifu, kina uhusiano wowote na hisia au la. Uchunguzi huo ndio uliotuwezesha kujibu swali la msingi lililoulizwa kuhusu ‘nini kinachofanya kijenzi husika kijirudie, yaani ujirudiaji hutagusana na nini?’

5.0 Muhtasari wa Tamthilia ya Ngoswe: *Penzi Kitovu cha Uzembe* kwa Kuzingatia Mwitiko wa Kitaharuki kwa Wahusika

Tamthilia hii ilichapishwa mwaka 1988 ikiwasilisha masuala anuwai kama vile mapenzi, uzembe kazini na kadhalika. Inaelezwa kwamba, Ngoswe, ambaye ni karani aliyetumwa na serikali ili kuhesabu watu, anajiingiza katika masuala ya mapenzi katikati ya jukumu alilopewa. Kujiingiza huko kunatokana na sababu kwamba mara amwonapo Mazoea, anaonesha kushtushwa na uzuri wa mwonekanao wake kiasi cha kuibua hisia za mapenzi. Hisia hizo zinamsukuma atumie juhudhi nyingi kumfuatilia Mazoea. Mama Mazoea anapobaini kitendo hicho, Ngoswe anashangaa kwa kuwa hakutarajia. Kutokana na mazingira ya nyumbani kumbana Ngoswe katika kukutana na Mazoea ili amweleze kuwa anamtaka kimapenzi, anaamua kumfuata Mazoea hadi mtoni alikoenda kuteka maji. Mazoea anapomwona Ngoswe aliyemfuta hadi mtoni, anaonesha taharuki kwa kushangaa kuhusu sababu iliyomleta kisimani. Hapo ndipo Ngoswe anafanikiwa kumweleza Mazoea kwamba anamtaka kimapenzi. Kwa hiyo, ili kutimiza azma hiyo, Ngoswe anamshawishi Mazoea kwamba wakati ukifika wa yeche kuhonda, awatoroke wazazi wake ili waondoke wote. Hata hivyo, wazazi wa Mazoea wanaonesha mwitiko wa kitaharuki baada ya kugundua Mazoea haonekani nyumbani mara baada ya Ngoswe kuondoka. Jambo hilo linawachochea kuanza kumtafuta Mazoea na hapo ndipo wanamwona akitoroka na Ngoswe. Ngoswe na Mazoea wanapotambua kuwa wanafuatiliwa, wanatimua mbio. Matokeo yake Ngoswe anadondosha mkoba wenye takwimu. Anapobaini kuwa amedondosha mkoba huo, Ngoswe anashindwa kuendelea na safari. Jambo hilo linamsukuma yeche na Mazoea warudi tena nyumbani kwa Mitomingi. Wanapofika nyumbani, Mitomingi anaduwaa kwa ujio wao. Aidha, kutokana na hisia za hasira, Mitomingi anaamua kuchoma takwimu zote. Ngoswe anapoona karatasi za takwimu zinateketea kwa moto, anaduwaa.

5.1 Uwasilishaji wa Data

Data ambazo zilikusanywa katika tamthilia ya Ngoswe: *Penzi Kitovu cha Uzembe* zinaonesha kwamba hisia zimejitokeza mara kwa mara kuitia taharuki za

wahusika kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 1: Ujitokezaji wa Hisia katika Tamthilia ya Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe

Dondoo lenye Mwitiko	Kujirudiarudia kwa Hisia	Ukurasa
<p>(...Akiwa ameinama akisoma, Mazoea binti kigori wa Mitomigi anakuja nyumbani kutoka mtoni huku amebeba ndoo ya maji. Asikiapo vishindo, <i>Ngoswe anainua macho kutazama. Aonapo kuwa ni msichana, anakoho na Mazoea akenua mdomo kidogo kwa tabasamu</i>⁵).</p> <p>Mazoea: Waonaje?</p> <p>Ngoswe: Salama dada (<i>Mazoea aingia ndani huku macho ya Ngoswe yakiwa mgongoni mwake. Atikisa kichwa na mara hiyohiyo Mitomigi na wazee wamili wanatokea...</i>)</p>	mapenzi, mshangao	2
<p>Mazoea: Hivi mama, huyu mgeni ametoka wapi?</p> <p>Mama Mazoea: Unauliza nini nawe. Hakuhusu! Unasikia?</p> <p>Mamainda: Usimsemeseme mtoto hivyo nawe!</p> <p>Kuuliza kutaka kujua kuna ubaya gani?</p> <p>Mama Mazoea: Baba yake unamjua ukali wake. Maswali kama hayo hayapendi...</p>	Hasira	3
<p>Mazoea: Hod! Hod!</p> <p>Ngoswe: Karibu.</p> <p>Mazoea: (<i>Anaingia</i>) Asante. Nimekuja kuchukua vyombo.</p> <p>Ngoswe: Vyombo! Kaa basi mbona unasimama kama vile hakuna viti.</p> <p>Mazoea: Nimeambiwa nifanye haraka.</p>	Woga	5
<p>Ngoswe: Leo akija hatoki mpaka tuelewane. Akiingia ni kufunga malango (<i>Mara asikia vishindo vya miguu. Anasimama na kujificha nyuma ya mlango. Asikia hod!</i>) Hod ya nini nawe Mazoea!</p> <p>Unaharibu sauti yako nyororo bure. Wewe ingia tu. (<i>Mama Mazoea aingiapo Ngoswe anagutuka.</i>)</p> <p>Shikamoo ma-ma.</p> <p>Mama Mazoea: Shikamo kutwa nzima mbona tumekwisha onana mara nyingi leo yote. (<i>Akiinama na kukusanya vyombo</i>). Haya nakwenda mwanangu. Lala salama.</p> <p>Ngoswe: (Hajibu kwa haya).</p>	mapenzi, woga, mshangao	12

⁵ Sehemu ya data yenye hati iliyokoza, ni msisitizo wa watafiti.

Mama: Sijui niwasaidie nini akina baba? Mitomingi: Mwenyewe yupo sijui? Mama: (<i>Akitazama chini mwenye huzuni anatingisha kichwa</i>) Hayupo. Mitomingi: Katoka kitambo? Mama: (<i>Akimtaazama Mitomingi kwa jicho kali</i>) Ni marehemu. Mitomingi: (<i>Amtazama Ngoswe ambaye kainamisha kichwa na wote wanatazamana kwa jicho la huruma</i>). Pole mama. Ngoswe: Pole mama...	huzuni hasira	13
Mitomingi: Kimya (Kwa hasira) Mama Mazoea, mwanao huyu mwangalie sana; sina zaidi...	hasira	18
Mama Mazoea: (<i>Akiokota</i>) Mtu wa watu kasahau kitabu chake. Hebu nimpelekee. (<i>Aelekea kibandani</i>). Hodi wenyewe. (<i>kimya</i>) Hodi (<i>Kimya. Hasikii jibu. Aingia na hakuti mtu. Astaaajabu</i> (<i>Aweka kitabu na kurudi jikoni</i>) Mamainda! Mamainda: Bee! Mama Mazoea: Mtu wa watu kaenda wapi? Mamainda: Yupi? Mama Mazoea: Huyu mgeni...	mshangao	20
(... <i>Ngoswe amekaa barazani akijisomea kitabu...Baada ya muda mfupi, Mazoea anatokea akiwa amebeba ndoo. Amwonapo Ngoswe pale nje akohoa na kuanza kuondoka huku akinengua. Ngoswe anaacha kusoma kitabu na kumtazama Mazoea mdomo wazi. Mazoea anapotoweka machoni, Ngoswe anayarudisha macho yake kitabuni lakini ashindwa kusoma...anza kufuata njia ya mtoni...</i>) (<i>Mazoea yu mtoni anateka maji. Mara anajiona amekamatwa kwa nyuma kiunoni. Anageuka kutazama</i>) Mazoea: (<i>Amwonapo Ngoswe</i>). Umenifuata mpaka huku? Ngoswe: Tena jee? (<i>Anamwachia na wanatazamana kwa muda. Mazoea anainama na kushughulika na kuchota maji</i>). Mazoea: Umefuata nini huku? Ngoswe: Nimefuata kinachofuatwa...	mshangao mapenzi	21

<p>Ngoswe: (<i>Anamtazama Mazoea kwa jicho la husuda</i>). Mpenzi Mazoea, nakupenda kifani sina.</p> <p>Mazoea: Kwa hiyo?</p> <p>Ngoswe: Tafadhali mpenzi usiniache nikateseka hivi. Nambie kama wanipenda.</p> <p>Mazoea: Sijui...Siwezi...Namwogopa baba.</p> <p>Ngoswe: Baba? Nini wewe? Kama wanipenda hutaogopa kitu. Unasikia? Penye nia pana njia sasa wasemaje?</p> <p>Mazoea: Sawa nakubali...</p>	mapenzi woga	22
<p>Ngoswe: ...Wajua nina jambo la muhimu kukueleza?</p> <p>Mazoea: (<i>Akichungulia mlangoni</i>) Liseme upesi.</p> <p>Ngoswe: Safari yetu sio kesho bali ni kesho kutwa asubuhi. Basi jitayarische. Unasikia?</p> <p>Mazoea: Nimesikia.</p> <p>(<i>Ni Alfajiri na mapema. Ngoswe amekwisha jitayarisha. Amejibanza kwenye migomba akimngojea Mazoea...Baada ya muda mfupi anamwona Mazoea akija kwa kunyata huku akibeba mzigo. Anafika Ngoswe anachukua mzigo...</i>)</p>	woga	25
<p>Mitomangi: Vipi! Mbona mwarudi?</p> <p>Ngoswe: Samahani mzee.</p> <p>Mitomangi: Kwani mmekosa nini?</p> <p>Ngoswe: Tumetoroka.</p> <p>Mitomangi: Kwani nani amewazuia? Tena ondokeni mbele yangu sitaki kuwaona. Hakuna mtu aliyewaambia mrejee hapa!</p> <p>Ngoswe: Lakini mzee hukunionea mzigo wangu wenye karatasi za takwimu?</p>	mshangao hasira	26
<p>Ngoswe: Basi mzee nisaheme mimi mwanao.</p> <p>Mitomangi: Mwizi hapati msamaha baba (<i>akimwambia Mama Mazoea</i>). Hebu niletee ukuni wa moto. (<i>Anayatoa makaratasi ya takwimu na kuyashika mkononi, ukuni wa moto waja</i>). Sasa kwa kuwa umeonyesha kuwa haya makaratasi huna haja nayo, mimi Ngengemkeni Mitomangi ninayachomelea mbali.</p> <p style="text-align: center;">...</p> <p>Mitomangi: (<i>Akianza kuyachoma</i>) Na ukijaribu kunisogelea ujue ndiyo kifo chako.</p> <p>Ngoswe: (<i>Akitazama karatasi zinapogeuka majivu kwa huzuni kuu</i>) Mungu wangu!</p> <p>Mitomangi: (<i>Akiyapuliza majivu yanapeperuka</i>) Hao watu wanaruka, wahesabu! (Ngoswe anatzama chini huku akitamani kulia...)</p>	hasira huzuni woga	27 na 28

Jedwali hili linaonesha mwitiko wa kimchomozo wa wahusika unaojitokeza kiuradidi, yaani kimotifu wenyewe kuchochewa na hisia.

5.2 Mjadala

Nadharia ya Rasa inaeleza kwamba mwitiko kama vile wa mshangao, ukali, tabasamu, maneno na matendo ya kimahaba, huzuni, kicheko, kilio, woga na kufanya jambo kwa kificho huashiria hisia fulani. Kwa kuongozwa na mawazo hayo ya Nadharia ya Rasa, data za utafiti zimeonesha kwamba miitiko ya kihisia imekuwa ikichomoza katika miktadha mbalimbali kwa kujirudiarudia. Mathalani, hisia za mapenzi zimejitokeza mara kadhaa hasa kupitia mhusika Ngoswe zinazomfanya amsake Mazoea ili atimize azma yake ya kimapenzi. Kwa mfano, Ngoswe amwonapo Mazoea kwa mara ya kwanza anaonesha mwitiko wa hisia za kimapenzi. Hisia hizo zinajirudia tena wakati mwingine pale Mazoea anapompelekea chakula chumbani kwake. Hapo Ngoswe anaonesha waziwazi na kuijiapiza kwamba mara Mazoea atakaporudi kuchukua vyombo, lazima atimize haja yake ya kimapenzi. Pamoja na azma ya Ngoswe kushindwa kutimizwa, hakati tamaa bali amwonapo Mazoea akielekea mtoni kuchota maji, anamfuata huko. Hatimaye, akiwa huko anamweleza habari za kumtaka kimapenzi na kumshawishi Mazoea awatoroke wazazi wake pamoja naye wakati wa kuondoka kwake.

Vilevile, Mazoea kwa nyakati tofautitofauti anaonesha hisia za woga hasa anapokuwa na Ngoswe na wazazi wake. Mathalani, kutokana na mama Mazoea kumkataza Mazoea asijaribu kujua habari za Ngoswe wala kujenga naye ukaribu, Mazoea anaonesha woga wa kumsikiliza Ngoswe akihofu kuwa endapo angekawia kurudi, huenda angejitumbukiza matatizoni. Kadhalika, Ngoswe anapomweleza kwamba anamtaka kimapenzi, Mazoea anatamka waziwazi kwamba hawezি kufanya maamuzi yoyote juu ya hilo kwa kuwa anamwogopa baba yake. Zaidi, Ngoswe anapotaka kumpa mpango wa safari ya kuwatoroka wazazi wake, kutokana na woga, kabla ya kusikiliza, Mazoea anachungulia kwanza kujiridhisha endapo hakuna mtu mwingine nje anayesikiliza maongezi yao. Naye Ngoswe anaonesha hisia za woga katika miktadha tofautitofauti. Kwa mfano, anapatwa na hisia za woga anapomwona mama Mazoea anaingia chumbani mwake kuchukua vyombo. Hii inajitokeza kufuatia pale anaposikia mtu anagonga mlango wake akidhani kuwa ni Mazoea; anamkaribisha kwa maneno ya utani kwamba asibishe hodi kwa sauti isiyovutia yenyewe kuharibu sauti yake nyororo. Ngoswe anayasema maneno hayo bila kujua kuwa anayekuja ni mama Mazoea. Hisia za woga kwa Ngoswe katika muktadha huu huenda zimesababishwa na mwangwi wenyewe kumjulisha mama Mazoea kwamba kuna jambo linaendelea baina ya wawili hao kinyume na matakwa yake. Aidha, kwa mara nyingine Ngoswe anapata hisia za woga pale anaporudi nyumbani kwa Mitomangi kuufuata mkoba wake wenyewe takwimu ulioanguka wakati akikimbizwa na wazazi wa Mazoea kwa sababu ya kumtorosha binti yao. Zaidi, Mitomangi anamtisha Ngoswe asijaribu kumsogelea wala kuchukua takwimu anazotaka kuziteketiza kwa moto kama kisasi dhidi ya

kitendo cha Ngoswe cha kudiriki kumwiba binti yao. Kutokana na hisia za woga, Ngoswe hathubutu kuokoa hata karatasi moja; badala yake, zote zinateketea kwa moto. Kwa hiyo, kujirudiarudia kwa hisia za woga mionganoni mwa wahusika kunaonesha kwamba hisia ni kipengele radidi, yaani motifu.

Aina nyingine ya mwitiko radidi imejitokeza kupitia mshangao kwa baadhi ya wahusika. Mathalani, mara tu Ngoswe amwonapo Mazoea anashangazwa kama msimulizi anavyotueleza kwamba binti huyo kigori anamvutia Ngoswe kiasi cha kuduwaan na kutikisa kichwa. Kadhalika, mwitiko wa mshangao unajitokeza kwa Ngoswe ambaye amepanga kwamba, mara tu Mazoea atakapokuja kuchukua vyombo, hatatoka mpaka waelewane. Hivyo, Ngoswe akidhani kuwa anayegonga mlango ni Mazoea, anamkaribisha kwa tambo huku akimwambia asibishe hodi kwa kuharibu sauti yake nyororo. Hata hivyo, anashangaa kumwona mama Mazoea akitokea badala ya Mazoea. Jambo hilo linamshangaza Ngoswe kiasi cha kumtia hisia za woga na kushindwa kuendeleza mazungumzo. Pia, Ngoswe anaonesha kushangazwa na mwonekano pamoja na mwendo wa Mazoea apitapo karibu naye. Msimalizi anaeleza kwamba mwendo wa Mazoea wa kunengua pia ulichangia Ngoswe apigwe na butwaa kiasi cha kuacha kusoma kitabu, kisha kumfuata mtoni. Kwa upande mwingine, kitendo cha Ngoswe kutoweka ghafla nyumbani kwa Mitomangi, kinamshangaza mama Mazoea hasa anapoona kitabu kimetelekezwa nje na Ngoswe haonekani katika mazingira ya nyumbani. Vilevile, Mitomangi anashangazwa na kitendo cha kurejea kwa Ngoswe baada ya kushindwa kuendelea na safari kutokana na kuangusha mkoba wenyе takwimu za sensa alipokuwa akimtorosha binti yake. Kwa ujumla, matukio mbalimbali katika matini teule yameonesha kuwashangaza wahusika kwa namna tofautitofauti. Suala hilo limeufanya mwitiko wa mshangao ujitokeze kiuradidi.

Katika matini teule, mwitiko mwingine wa wahusika ulioonekana kujitokeza kwa kujirudiarudia ni hasira. Data zimeonesha kwamba wahusika huonesha mwitiko wa hasira hasira linapotokea jambo wasilolipenda. Mathalani, kwa kuwa mama Mazoea hapendi bintiye Mazoea ajue habari za Ngoswe wala kuwa karibu naye, anaonesha hasira kwa kumfokea Mazoea anapouliza habari za Ngoswe. Mhusika mwingine anayeonesha hisia za hasira ni mama mjane ambaye hatajwi jina mahususi. Huyu, kutokana na kufiwa na mume wake, anapatwa na hisia za hasira hasa makarani wa sensa wanapomuulizauliza mahali alipo mume wake wasijue kuwa alishaaga dunia muda mrefu uliopita. Naye Mitomangi anaonesha kuwa na hasira hasa anapodhani kuna jambo linaendelea kwa kificho baina ya Mazoea na Ngoswe ambalo ye ye halipendi. Huenda hasira za Mitomangi zinasababishwa na suitafahamu kuhusu mienendo ya Mazoea ilhali akijua tayari sehemu ya posa imeshapokelewa ya kumwoza Mazoea kwa mwanamume mwingine ambaye si Ngoswe. Vilevile, Mitomangi anaonesha hasira kutokana na kitendo cha Ngoswe kumtorosha binti yake. Kutokana na purukushani za kumwokoa Mazoea, Mitomangi anaokota mkoba wa Ngoswe wenyе takwimu, kisha kuzichoma karatasi

zote zenye takwimu. Jambo hilo pia linaibia hisia za hasira kwa Ngoswe kwa kuwa hakupenda kitendo hicho kifanywe.

Kadhalika, kitendo cha upotevu wa kile kinachothaminiwa kimewafanya wahusika wahuzunike. Mathalani, mama aliyefiwa na mume wake anahuzunika hasa apokumbushwa habari zake na makarani wa sensa. Kwa kuwa Nadharia ya Rasa inaeleza kuwa hisia hujitokeza katika hali ya mtoano, hii inaonesha kuwa hisia za huzuni zilisababishwa na hisia za hasira. Kadhalika, makarani nao wanapotambua kuwa wanayemuulizia hayupo duniani, wanaungana kuhuzunika pamoja naye. Simulizi pia inaonesha kwamba Ngoswe anapoona kazi iliyofanywa kwa ugumu inaharibiwa mbele ya macho yake, anahuzunika. Hali hii inaonesha kwamba wahusika wameonesha mara kadhaa kuhuzunika kutokana na kuwapo kwa jambo baya.

Kwa hiyo, kutokana na uchambuzi wa data uliofanywa, matokeo ya utafiti hayaoneshi kупingana na tafiti tangulizi kama ilivyotangulia kuelezwaw kwamba, wanazuoni hawahitilafiani kuhusu msingi wa utambuzi wa motifu kuwa ni uradidi wa kipengele husika. Mathalani, katika data imeonekana kwamba hisia hasa za mapenzi ndizo zilizosababisha safari za mara kwa mara baina ya Ngoswe na Mazoea. Jambo hili limeonesha kwamba safari ni mhimiili wa kuibua motifu katika tamthilia ya *Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe*. Matokeo haya yanaelekeana na mawazo ya wataalamu kama Lubbungu (2011) aliyeleza kwamba mhusika anapopata wazo jipya ambalo ana uhakika kwamba utekelezaji wake utampa mafanikio au majibu ya maswali yake; hapo ndipo huanza safari ya kusaka jambo husika. Kwa kuwa utimizaji wa matamanio mengi katika jamii huhitaji kuweka juhudhi fulani kama inavyoelezwa na Daemrich (1997), huenda hii ndio sababu inayofanya motifu ya safari kupewa kipuamble zaidi kiutungaji, uwasilishaji na uchambuzi katika matini za kifasihi. Mathalani, katika uchambuzi jambo hili linajitokeza kupitia tafiti za wanazuoni waliochambua kuhusu motifu ya safari kama vile: Senkoro (1997), Daemrich (1997), Lubbungu (2011), Mulokozi (2017), Lema (2018) na Mung'aya (2018).

Kwa hiyo, matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba hisia na safari ni kama pande mbili za sarafu ambazo hukamilishana. Mathalani, mara tu Ngoswe anapomwona Mazoea, ambaye kwa mujibu wa Nadharia ya Rasa, anaibua hisia za mapenzi ambazo zinamshughulisha kufanya safari kadhaa za kumsaka Mazoea ili amweleze azma yake. Ngoswe anaonesha nia ya kumsaka akiwa chumbani kwake, kisimani, na hata kudiriki kutoroka naye. Kwa hiyo, ndani ya msako huo ndipo kunaibuka hisia za hasira, mshangao, huzuni na kadhalika. Kama ilivyokwisha kuelezwaw na wataalamu kama Lubbungu (2011) kwamba kuna aina mbalimbali za safari kama vile ya kijiografia na kisaikolojia; kadhalika, matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba kwa kiasi kikubwa safari anazofanya Ngoswe ni za kijiografia na kisaikolojia ambazo huchochewa na hisia zinazomfanya amsake Mazoea. Kijiografia kwa sababu anaondoka kutoka eneo moja kwenda jingine na

pia ni za kisaikolojia kwa kuwa hata akiwa ametulia, anaendeleza mipango ya kumsaka Mazoea.

Kadhalika, wataalamu wanaeleza kwamba mionganoni mwa sababu za watanzi wa matini husika kuwasilisha kipengele husika kwa kujirudiarudia ni kusitiza juu ya wazo linalobebwa kwenye kipengele husika (Daemmrich, 1997; Senkoro, 1997; Lubbungu, 2011; Morgan, 2015; Mulokozi, 2017). Jambo hilo linaonesha kwamba upo uhusiano wa karibu baina ya motifu na maudhui (dhamira) kama inavyoiezwa bayana na Daemmrich (1997), Senkoro (1997), Lubbungu (2011), Morgan (2015), Mulokozi (2017) na Lema (2018). Hali hiyo, inaonesha kwamba kipengele husika kinapojitokeza kwa kujirudia, humchochea mchambuzi kutafuta maana iliyobebwa kwenye kipengele husika (Mutembei, 2012). Mathalani, mionganoni mwa dhamira ambazo mwangwi wake unajengwa kiuradidi kupidia hisia ni suala la mapenzi ambalo ndilo limebeba anwani ya matini iliyochambuliwa, yaani *Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe*. Jina hilo la kitabu linaonesha kwamba maudhui yanayowasilishwa kwa kiasi kikubwa yanahusu suala la mapenzi.

Hivyo, kutokana na matokeo ya utafiti kuonesha uhusiano baina ya motifu na hisia, swali la msingi liloulizwa mwanzoni mwa matini hii linabaki kuwa kwa nini wachambuzi wa motifu hawajaweka bayana ukaribu wake na hisia? Jibu la swali hili linaweza kutokana na sababu mbalimbali. Mionganoni mwazo ni kwamba, huenda ni kutokana na athari za mawazo ya baadhi ya wataalamu kama vile Mohamed (1995), Brecht (1957), Mounce (1980), Kezilahabi (1993) na Boal (2008) wanaoleza kwamba hisia ni dhana telezi jambo linalosababisha ugumu katika uchambuzi wake.

Kwa maoni yetu, mtazamo kwamba hisia ni telezi ni wa jumla mno, yaani mtazamo huo umetoa mahitimisho bila kutazama hisia katika muktadha mahususi wa matini husika kiuchambuzi. Hii ni kama inavyoiezwa na Mnenuka (2017) kwamba ikiwa kila dhana au jambo litatazamwa katika muktadha wake, hakuna utata wa kulishughulika jambo husika. Kwa hiyo, data zilizowasilishwa zinaonesha kwamba msingi huohuo unaotumika kubainisha motifu kama vile ya safari, ndio umejitokeza kupidia hisia za wahusika. Kwa mantiki hiyo, katika makala haya tunajenga hoja kwamba, hisia zinatagusana na hali ya kujirudiarudia kwa jambo kiasi cha kuzifanya kuwa mionganoni mwa kichocheo katika uibuzi wa motifu kama vile motifu ya safari inayohusisha msako wa masuala kama vile mapenzi, motifu ya hasira, motifu ya woga, motifu ya mshangao, na motifu ya huzuni.

6.0 Hitimisho

Data zilizowasilishwa zinaonesha kwamba msingi wa ujitokezaji wa hisia ni kuwapo kwa mwitiko wa kimchomozo. Jambo hilo linaonesha kwamba kujirudiarudia kwa mwitiko wa kimchomozo ndiko kunakoibua motifu na kwamba

hisia ni mionganini mwa vichocheo vya kuwapo kwa motifu. Kadhalika, matokeo yameonesha kwamba, ikiwa hisia zitatazamwa katika matini kwa kuzingatia muktadha wa ujitokezaji wake, ni wazi kwamba si telezi. Kwa mantiki hiyo, hoja ya makala haya ni kwamba motifu na hisia hutagusana kwa kuwa hutegemena na kukamilishana katika ujitokezaji wake.

7.0 Marejeleo

- Abrams, M.H. (1953) *The Mirror and the Lamp: Romantic Theory and the Critical Tradition*. Oxford: Oxford University Press.
- BAKITA (2022) *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la 3). Dar es Salaam: Longhorn Publishers.
- Benjamin, S. (2012) “On the Distinctiveness of Poetic Language”. *New Literary History*. Juz. 43 (1): 89-111. Inapatikana katika <https://www.jstor.org/stable/pdf/23259362.pdf>. Ilisomwa tarehe 24/06/2024.
- Boal, A. (2008) *Theatre of the Oppressed*. London: Pluto Press.
- Daemmrich, I.G. (1997) *Studies on Themes and Motifs in Literature*. New York: Peter Lang.
- Semzaba, E. (2006) *Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe*. The General Booksellers Ltd. Dar es Salaam.
- Haldane, J.B.S. (1992) “Animal communication and the origin of human language”. *Current Science*. Juz. 63 (9/10): 604-611. Inapatikana katika <https://www.jstor.org/stable/pdf/24094586.pdf>? Ilisomwa tarehe 24/06/2024.
- Hogan, P.C. (2011) *What Literature Teaches us About Emotion*. New York: Cambridge University Press.
- Kezilahabi, E. (1993) “Dhana ya Uhuru wa Mwandishi”. Katika M.M. Mulokozi na C.C. Mung’ong’o (wh). *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam: DUP. kur. 13-18.
- Leech, G. (2008) *Language in Literature: Style and Foregrounding*. New York: Taylor and Francis Group.
- Lema, E.P. (2018) “The Journey Motif and the Re-Reading of Ngugi wa Thiong’o: *Devil on the Cross*, *Matigari* and *Wizard of the Crow*, A Gikuyu Trilogy”. *Utafiti*, Juz. 13(2): 173-191.
- Lubbungu, J. (2011) “The Significance of Journeys in the Novels of Oyono, Ngugi and Eliot: A study of Old Man and the Medal, Devil on the Cross and Silas Marner”. Inapatikana katika <https://www.academia.edu/26933697/> Ilisomwa tarehe 17 Oktoba 2023.
- Lubbungu, J. (2016) “Does the Number Three (3) Mean Anything in James Joyce’s “A Portrait of the Artist as a Young Man”? *International Journal of Arts & Sciences*. Juz. 9(4): 283–290. Inapatikana katika <https://www.researchgate.net/publication/349863822>. Ilisomwa tarehe 20 Juni 2024.
- Mbenna, I.C. (1970) *Uandishi wa Vitabu*. Dar es Salaam: TPH.

- Mnenuka, A.J. (2017) *Exploring Modernity in African Overture: The Bena Case Study*. Tazimili ya Uzamivu. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Leipzig, Leipzig. Inapatikana katika <https://core.ac.uk/download/pdf/226126924.pdf>. Ilisomwa tarehe 05-19 Januari 2024.
- Mohamed, S.A. (1995) *Kunga za Nathari za Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishes Ltd.
- Mounce, H.O. (1980) "Art and Real Life". *Philosophy*. Juz. 55(212): 183-192.
- Mulokozi, M.M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Mutembei, A.K. (2012) *Korasi katika Fasihi*. Dar es Salaam: TUKE.
- Rasa Theory. Ilisomwa kupitia <https://egyankosh.ac.in/bitstream/123456789/35508/1/Unit-.pdf>.
- Semzaba, E. (1988) *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe*. Dar es Salaam: The General Booksellers Ltd.
- Senkoro, F.E.M.K. (1997) *The Significance of the Journey in Folk Tales from Zanzibar*. Tazimili ya Uzamivu. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Sosoo, F.K. (2019) "Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa katika Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania". *Mulika*. Juz. 38: 1-25.
- van Dijk, T.A. (2008) "Text, context and knowledge". Imesomwa kutoka <https://www.semanticscholar.org/paper/Text-%2C-context-and-knowledge>.
- wa Mutiso, K. (2012) "Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili". *Mulika*. Juz. 31: 115-135.
- Willett, J. (mh.) (1957) *Brecht on Theatre: The Development of an Aesthetic*. Daryagan: Radha Krishna.